

# HALMASHAURI YA WILAYA MASASI

(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Simu: 023 - 2510013, 2510031.  
Fax: 023 - 2510214, 2510652, 2510752  
E-mail: ded@masasi.go.tz  
infor@masasi.go.tz



S.L.P. 60,  
Masasi,  
Mtwara,  
TANZANIA.

---

## YAH: TAARIFA KWA UMMA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi anapenda kuwataarifu wananchi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kuwa **Mwenge Wa Uhuru** utakimbizwa tarehe **14, Mei, 2017** katika halmashauri hiyo.

Mwenge wa uhuru utapokelewa katika kijiji cha Nanyindwa na utakimbizwa kwenye kata za Chiwale, Mpanyani, Lukuledi, Chikunja, Mpindimbi, Chiwata, Chigugu, Chikundi, Mwena na Ndanda. Hivyo wananchi wote wa maeneo hayo mnaombwa kushiriki katika mapokezi ya mwenge wetu wa Uhuru kwa kuushangilia na kusikiliza ujumbe pindi utakapo pita katika maeneo yenu.

Mbio za mwenge wa uhuru mwaka huu wa 2017 una kaulimbiu isemayo ***"shiriki katika uchumi wa viwanda kwa maendeleo ya nchi yetu"***

Mwenge wa uhuru ukiwa halmashauri ya wilaya ya masasi utakagua na kuzindua miradi mitano (5) yenye thamani ya shilingi Bilioni **2,040,128,341**.

Mwenge utapoelewa katika kijiji cha Nanyindwa kilichopo kata ya chiwale na mkesha wa mwenge utafanyika kata ya Ndanda, wananchi wote mnakaribishwa.

Imetolewa na:

**Joina J. Nzali**  
**Afisa Habari**  
**Halmashauri ya Wilaya ya Masasi**

